Tumeitwa Kuwa Watu Wakubwa

na

Ellis P. Forsman

Tumeitwa Kuwa Watu Wakubwa

na

Ellis P. Forsman

Novemba 5, 2011

Tumeitwa Kuwa Wanaume Wakubwa

(Na Wanawake Wakubwa, pia)

Mapema katika karne iliyopita kitabu kilichopewa jina “Mtu mkubwa” kili haririwa na mtu mmoja maarufu daktari wa akili. Kusudi la kitabu ilikuwa ni, kupitia “badiliko” watu wangeweza kuwa na akili zenye kuona mbali na kimwili kwamba wakati wa baadaye wa (mwanadamu) ungeweza kujitakasa katika mikono yake. Hii ilianzisha hitaji la “Uwezo wa kuwepo”.

Baadaye katika karne, mtu mmoja maarufu wa jina kama hilo ilo akawa maarufu, pamoja na video na matoleo ya televisheni. Hii ilikuwa ni dhahiri.

Kama Wakristo, tumeitwa kuwa “watu wakubwa” na “wanawake wakubwa”. Hii ikowazi na haijakosewa kutoka katika kusoma maandiko.

“MKUU” – “Juu…ya kiwango cha juu, uwezo nk. Kwa kiwango hasa cha juu.”

- Siyo kitabu cha ushindi kilicho na “uwezo wa hali ya juu”.
- Siyo wazo la Niezsche lenye undaji wa hali ya juu, kuhamisha, nk.
- Siyo uwezo mkuu wa mwanadamu “badiliko”.
- Siyo ushurutishwaji wa wenye uwezo, nguvu au ulazima wa matakwa.

Kama siyo hivi vitu, ni uwezo “mkuu” wa aina gani tunatakiwa tuwe?

- “KAMILIFU” – “Hali ya kuwa au kufanyika kamili”
- “Ukamilifu wa ujumla au mfano wa kitu Fulani”
- “Ubora au tabia au uwezo wa hali ya juu ya ukamilifu”
- “kitendo au ukweli wa kukamilika na kumalizika”

Agizo la kuwa "Kamili" Inaashiria Uwepo Wa Kutokukamilika.

Sisi Sote ni wenye Dhambi

- Yohana 16:8, "*Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.*"
- Waru. 3:9, "*… kwa maana tumekwisha kuwashitaki Wayahudi na Wayunani ya kwamba pia wamekuwa chini ya dhambi;*"
- Waru. 6:17, "*…mlikuwa watumwa wa dhambi…*"
- Waru. 6:23, "*…mshahara wa dhambi ni mauti…*"
- Wagal. 3:22, "*Lakini andiko imeyafunga yote chini ya nguvu ya dhambi…*"
- 1 Yohana 1:8, "*Tukisema kwamba hatuna dhambi twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu.*"

Hivyo tumeonyeshwa dhahiri kuwa sisi ni viumbe wenye makosa, walio na dhambi; zaidi sana tumetokea kuharibu Sheria ya Mungu, ambayo ni dhambi kubwa zaidi ya yote.

Je! Tunawezaje Kutarajia Kuwa Kamilifu?

Tumeagizwa kuwa "wakamilifu".

- Math. 5:48, "*Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.*"
- Luka 6:40, "*Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake.*"
- 2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

Kamilifu Katika Nini?

Katika Umoja.

- Yohana 17:23, "*…ili wawe wakamilifu katika umoja…*"
- Waef. 4:13, "*Hata na sisi sote tutakapoufikia… mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.*"

Katika Saburi.

Yakobo 1:4, "*Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.*"

Kujizuia.

Yakobo 3:2, "*Maana twajikwaa sisi sote pia katika mambo mengi. Mtu asiyejikwaa katika kunena huyo ni mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote, kama kwa lijamu.*"

Katika Upendo.

1 Yohana 4:16-17, "*Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi na kuliamini. Mungu ni pendo naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu na Mungu hukaa ndani yake. Katika hili pendo limekamilishwa kwetu ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu.*"

(Inaondoa hofu) 1 Yohana 4:18, "*Katika pendo hamna hofu, lakini pendo lililokamili hulitupa nje hofu…*"

Katika Udhaifu.

2 Wakor. 12:9, "*...Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu...*"

Viumbe Ambavyo Siyo Kamili Viwe Kamili?

Tumeona kwa sisi ni viumbe ambavyo havijakamilika, na kwa wakati huo huo tunaagizwa kuwa "kamili". Tunawezaje kuelewa mkanganyiko huu uliowazi? Kama ilivyo kila mara, maandiko yanatoa jibu!

Kuwa katika Kristo. Yohana 15:4, "*Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu.*"

Vivyo hivyo kama vile chombo hakiwezi kufanya kazi kama ikiondolewa katika chanzo chake cha moto, hivyo na sisi, kama tukiondolewa katika chanzo chetu, hatuwezi kupata "ukamilifu".

Chanzo chetu cha nguvu ni nini? Waru. 1:16, "*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye…*"

Kristo hakuwa na dhambi. 1 Petr. 2:21-22, "*Kwa sababu ndiyo mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake. Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake.*"

Ukamilifu Ni Utimilifu.

Katika yote haya, hatupati wazo kwamba Bwana wetu au Mitume wake walifundisha kwamba wokovu inategemea katika hali ya kupata ukamilifu (hiyo ni, kutokuwepo makosa au dhambi), kwa sababu hiyo haijafundishwa popote katika maandiko. Kile ambacho neno inamaanisha ni "utimilifu". Bwana anatutaka tuwe "wakamilifu" (tumetimilika) tukisimama katika imani ya injili. Katika njia hii, tunaweza kukaa katika mafundisho ya Mtume Paulo katika 2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*" Na tena katika 2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

Kwa juhudi zetu za kukidhi uwezo wa maisha yetu kwa muunganiko na chanzo chetu cha nguvu, tunaweza "kufanya kila tendo jema". Huu ndiyo ukamilifu tunaoweza kupata.

Kushindania Ukamilifu.

Paulo, aliyetufundisha kuwa "wakamilifu", anayaweka yote katika mtazamo katika barua yake kwa Wafilipi, Wafil. 3: 12-14, "*Si kwamba nimekwisha kufika au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. Ndugu sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma , nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo niifikie mede ya dhawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.*"

Si mmoja wetu atakaye pata uwepo wa "ukamilifu" katika maisha haya, lakini tunaweza kufanya kama Paulo alivyotowa mukhutasari katika kauli yake hapo juu katika msitari wa 15, "*Basi sisi tulio wakamilifu na waze hayo; na hata mkiwaza mengine katika jambo lo lote, Mungu atawafunulia hilo nalo.*"

Ni tumaini langu kwamba wote tutashindania ukamilifu katika ujuzi wa neno la Mungu na kujishikilia sisi wenyewe kufanya kila tendo jema katika Kristo Yesu.

Ndugu yenu katika Kristo,

J. D. Logan

-